# JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

## WIZARA YA KILIMO

## BODI YA KOROSHO TANZANIA

**MWONGOZO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO ZA RUZUKU KWA WAKULIMA WA KOROSHO NCHINI MSIMU WA MWAKA 2024/2025**

***Mwongozo huu umetolewa chini ya Sheria ya Tasnia ya Korosho***

***Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010***

**Umetayarishwa na:-**

*Bodi ya Korosho Tanzania,*
*S. L. P 533,*
***MTWARA.***

**Aprili, 2024**

## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ..... 5
2.0 MWENENDO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO NA UZALISHAJI WA KOROSHO NCHINI ..... 5
3.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO ..... 7
4.0 MBINU ZILIZOTUMIKA KUTAYARISHA MWONGOZO ..... 7
5.0 UPATIKANAJI WA PEMBEJEO MSIMU WA 2024/2025 ..... 7
6.0 UDHIBITI WA UBORA WA PEMBEJEO ..... 8
7.0 GHALA KUU ZA PEMBEJEO ..... 8
8.0 USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO ..... 9
9.0 MFUMO WA KIDIJITALI WA UGAWAJI WA PEMBEJEO ..... 9
10.0 USAJILI WA VITUO VYA KUGAWA PEMBEJEO ..... 9
10.1. UTARATIBU WA UGAWAJI WA PEMBEJEO ..... 9
10.2. Usajili/Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Korosho ..... 10
10.3. Mgao na Ugawaji wa Pembejeo kwa Wakulima ..... 10
11.0 JINSI MFUMO WA KIDIJITALI UTAKAVYOFANYA KAZI ..... 11
12.0 UTOAJI WA ADHABU ..... 12
13.0 USIMAMIZI, UFUATILIAJI NA TATHMINI ..... 12
13.1. Muundo wa Kamati ya Kitaifa ..... 12
13.2. Muundo wa Kikosi Kazi cha Mkoa ..... 13
13.3. Muundo wa Kikosi Kazi cha Wilaya ..... 13
14.0 UGHARAMIAJI KWA WANAOHUSIKA NA USIMAMIZI NA UFUATILIAJI ..... 13
15.0 UGHARAMIAJI WA SHUGHULI ZA USAMBAZAJI NA UGAWAJI ..... 13
16.0 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO ..... 14
17.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU ..... 14
17.1. Wizara ya Kilimo ..... 14
17.2. Kikosi Kazi cha Mkoa ..... 14
17.3. Bodi ya Korosho Tanzania ..... 15
17.4. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ..... 15
17.5. Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) ..... 16
17.6. Vyama Vikuu vya Ushirika ..... 16
17.7. Vyama vya Ushirika vya Msingi ..... 17
17.8. TARI Naliendele ..... 17
17.9. KCJEL Ltd ..... 18
17.10. Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania ..... 18
17.11. Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Pembejeo za Ruzuku za Korosho ..... 18
17.12. Kikosi Kazi cha Wilaya ..... 19
17.13. Wazabuni wa Pembejeo ..... 19
17.14. Mkulima wa Korosho ..... 20
17.15. Taasisi za Fedha ..... 20
17.16. Waandishi wa Habari ..... 20
18.0 WAJIBU WA PAMOJA ..... 20
19.0 MUDA WA UTEKELEZAJI ..... 21
20.0 ILANI ..... 21
21.0 HITIMISHO ..... 21

## TAFSIRI YA BAADHI YA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika Mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| **"CORECU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Mkoa wa Pwani. |
| **"KCJE Ltd"** | Kampuni iitwayo Korosho Cooperative Joint Enterprise Limited iliyoanzishwa na Vyama Vikuu vya Ushirika MAMCU Ltd, TANECU Ltd, TAMCU Ltd, CORECU Ltd, RUNALI na LMCU kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo, mabomba na magunia na kusambaza kwa wakulima nchini. Kampuni hiyo imesajiliwa kwa jina la. |
| **"LMCU"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Lindi na Kilwa (Lindi Mwambao). |
| **"MAMCU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Mtwara, Masasi na Nanyumbu mkoa wa Mtwara. |
| **"Mwongozo"** | Mwongozo wa upatikanaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba katika zao la korosho nchini kwa msimu wa mwaka 2024/2025 unaotolewa chini ya sheria ya tasnia ya korosho na. 18 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2010. |
| **"RUNALI"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale. |
| **"Sheria"** | Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009. |
| **"TACACU"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Mkoa wa Tanga. |
| **"TAMCU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya ya Tunduru. |
| **"TANECU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Newala na Tandahimba mkoa wa Mtwara. |
| **"TPHPA"** | Tanzania Plant Health and Pesticides Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania). |
| **"Wazabuni"** | makampuni yaliyoshinda zabuni kusambaza pembejeo, Magunia na Mabomba nchini ambayo yamefunga mkataba na Kampuni ya **KCJE Ltd** kwa ajili hiyo. |
| **CBT** | Cashewnut Board oa Tanzania - Bodi ya Korosha Tanzania |

# DIBAJI

Zao la korosho ni mojawapo ya mazao makuu ya biashara nchini yanayoliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya mwaka 2021/2022 korosho iliongoza kwa kuchangia Dola za Marekani milioni 159 ikifuatiwa na kahawa, tumbaku na pamba. Kwa kuzingatia umuhimu huu, katika msimu wa mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kusambaza pembejeo na mabomba ya ruzuku kwa wakulima. Lengo la mpango huo ni kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi na hatimaye kuleta manufaa ya kipato kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Utayarishaji wa mwongozo huu umejumuisha maoni ya wadau katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini ikiwemo Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya, Taasisi za Serikali, Vyama vya Ushirika na Wakulima. Aidha, Sera, Mikakati na Mipango ya Taifa iliyozingatiwa katika maandalizi hayo ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa *(Tanzania Development Vision - TDV 2025)*; Mpango wa Taswira ya Muda Mrefu wa Taifa *(Long Term Perspective Plan -LTPP 2012-2021)*; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(Third Five Year Development Plan - FYDP III 2021/22-2025/26)*; Sera ya Taifa ya Kilimo ya 2013; Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 2002; Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agricultural Sector Development Program Phase II – ASDP II 2017/18 - 2027/28)*; Mkakati wa Tasnia ya Korosho Nchini 2013/2014 – 2024/2025 *(Cashewnut Industry Strategy 2013/2014 – 2024/2025)* na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Aidha, Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya 2009 *(The Cashewnut Industry Act No. 18, 2009)*, Sheria ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Na. 4 ya 2020 imezingatiwa.

Vilevile, Mwongozo huu umezingatia mipango na programu za kikanda na kimataifa zinazohusu sekta ya kilimo ikiwemo Programu Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Afrika *(CAADP, 2015-2025)*; Malengo ya Maendeleo Endelevu *(Sustainable Develepment Goals-SDGs)* pamoja na itifaki na mikataba mbalimbali ambayo nchi imeridhia kuhusu matumizi salama ya viuatilifu kwa afya ya wanyama, mimea na mazingira (Mkataba wa Rotterdam na Stockholm).

Pia, Mwongozo huu umezingatia vipaumbele vya Wizara ya Kilimo ambavyo ni kuongeza tija na kuweka mkazo kwenye utafiti utakaozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo; kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora; kuimarisha huduma za ugani; kuimarisha kilimo

cha umwagiliaji; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo; kuimarisha kilimo anga kwa ajili ya kudhibiti visumbufu; na kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji.

Hivyo, ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa shirikishi na utaleta manufaa yaliyokusudiwa kwa wadau wote katika Tasnia ya Korosho hapa nchini.

Natanguliza shukrani kwa ushirikiano wenu.

Francis Alfred
**MKURUGENZI MKUU**
Tarehe 18 / 04 /2024

## 1.0 UTANGULIZI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya, Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini, wakulima na wadau wengine wanaendelea na maandalizi ya uzalishaji wa korosho msimu wa mwaka 2024/2025. Katika msimu wa mwaka 2024/2025 kama ilivyokuwa msimu wa mwaka 2023/2024, Serikali itatoa ruzuku kwenye pembejeo na mabomba yatakayosambazwa na Vyama Vikuu vya Ushirika kwa wakulima. Ruzuku hiyo ni sehemu ya mahitaji ya mkulima kwa lengo la kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji wa korosho hapa nchini. ***Kwa muktadha huo kila mkulima anakumbushwa kuweka akiba ya fedha kwa ajili ya kununua viuatilifu sokoni ili kukidhi mahitaji yake.***

## 2.0 MWENENDO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO NA UZALISHAJI WA KOROSHO NCHINI

Pembejeo za kilimo cha korosho hususani viuatilifu na mabomba katika zao la korosho ni muhimu ili kuwawezesha wakulima kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi nchini. Kwa misimu ya nyuma kabla ya msimu wa mwaka 2018/2019, Serikali ilitoa ruzuku ya asilimia hamsini (50%) ya pembejeo na mabomba isipokuwa msimu wa 2017/2018 ambapo pembejeo zilitolewa bila malipo kwa wakulima. Kuanzia msimu wa mwaka 2018/2019, Serikali haikutoa ruzuku na hivyo wakulima walijigharamia kwa kujipatia pembejeo na mabomba kutoka kwa wasambazaji waliokuwepo sokoni. Wakulima walinunua pembejeo hizo kwa fedha taslimu au mkopo ambao hata hivyo urejeshaji wake ulikuwa siyo wa kuridhisha. Mathalani; msimu wa 2018/2019 hadi msimu wa 2020/2021 Bodi ya Korosho Tanzania, Vyama Vikuu vya Ushirika na Mabenki walikopesha pembejeo kwa wakulima na mikopo hiyo haikuweza kurejeshwa kwa wakati.

Utaratibu wa wakulima kujigharamia pembejeo ulionekana kutoleta matokeo yaliyokusudiwa. Hii ni kutokana na wakulima wengi kutokuwa na fedha za kununua pembejeo za kutosha kudhibiti visumbufu vya zao la korosho. Kumbukumbu zilizopo Bodi ya Korosho Tanzania zinaonesha kuwa uzalishaji wa korosho ghafi nchini ulipungua kutoka tani 313,826 msimu wa 2017/2018 hadi tani 210,787 msimu wa 2020/2021 kutokana na wakulima kushindwa kudhibiti visumbufu vya zao la korosho.

Uamuzi wa Serikali kurejesha mfumo wa ruzuku kwenye pembejeo na mabomba katika zao la korosho nchini kuanzia msimu wa 2021/2022 uliwezesha uzalishaji wa korosho ghafi kuongezeka kutoka tani 210,787 msimu wa 2020/2021 hadi tani 305,000 msimu wa 2023/2024 sawa na ongezeko la 45%. Jedwali Na. 1 linaonesha mwenendo wa matumizi ya pembejeo na uzalishaji wa korosho ghafi nchini kuanzia msimu wa 2012/2013 hadi msimu wa 2023/2024.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa Matumizi ya Pembejeo na Uzalishaji wa Korosho ghafi Nchini kuanzia Msimu wa 2012/2013 hadi Msimu wa 2022/2023.**

| Msimu | Viuatilifu vya Maji | Sulphur ya Unga (Tani) | Uzalishaji wa Korosho Ghafi (Tani) |
|---|---:|---:|---:|
| 2012/2013 | 182,230 | 5,000 | 127,947 |
| 2013/2014 | 346,300 | 5,000 | 129,823 |
| 2014/2015 | 300,000 | 8,000 | 198,114 |
| 2015/2016 | 160,000 | 10,000 | 155,245 |
| 2016/2017 | 255,000 | 15,000 | 265,238 |
| 2017/2018 | 310,000 | 18,000 | 313,826 |
| 2018/2019 | 339,009 | 12,352 | 225,154 |
| 2019/2020 | 448,258 | 8,610 | 232,682 |
| 2020/2021 | 182,438 | 8,731 | 210,787 |
| 2021/2022 | 1,497,354 | 13,562 | 240,158 |
| 2022/2023 | 2,683,682 | 15,014 | 187,849 |
| 2023/2024 | 1,989,238 | 39,275 | 305,000 |

***NB:** Msimu wa 2023/2024 takwimu za uzalishaji wa korosho ghafi ni kwa mujibu taarifa zilizokusanywa hadi tarehe 15 Aprili, 2024. Ukusanyaji wa taarifa bado unaendelea hususani kutoka Mikoa Mipya na baadhi ya Wilaya za Mikoa ya Asili ambako wakulima wanabangua na kuuza korosho zilizobanguliwa.*

### 3.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO


Madhumuni ya mwongo huu ni Kutoa maelekezo juu ya utaratibu wa usambazaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima wa korosho msimu wa 2024/2025 ikiwa ni pamoja na kuanisha majukumu ya kila mdau kwenye zoezi hilo.

### 4.0 MBINU ZILIZOTUMIKA KUTAYARISHA MWONGOZO

Mbinu mseto zimetumika katika kufanikisha maandalizi ya Mwongozo huu ikiwa ni pamoja na mapitio ya Mwongozo uliotumika msimu wa mwaka 2023/2024 sanjari na ushirikishaji wa taasisi za umma na zile za binafsi pamoja na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini zikiwemo Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Kituo cha Naliendele - TARI Naliendele; Mamlaka ya Usimamizi wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA); Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC); Vyama Vikuu vya Ushirika *(Unions)* na Kampuni ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika (KCJEL). Hivyo, ni matumaini ya Serikali kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa shirikishi na utaleta manufaa yaliyokusudiwa na wadau wa Tasnia ya Korosho hapa nchini.

### 5.0 UPATIKANAJI WA PEMBEJEO MSIMU WA 2024/2025

Kielelezo hapa chini kinaonesha Mfumo wa upatikanaji wa pembejeo hadi ngazi ya mkulima;




**Kielelezo Na. 1: Mfumo wa upatikanaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho nchini hadi ngazi ya mkulima.**

Pembejeo za ruzuku za zao la korosho kwa ajili ya msimu wa 2024/2025 zimeagizwa na Kampuni ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika ijulikanayo kwa jina la KCJE Ltd (yaani Korosho Cooperative Joint Enterprise Limited). Vyama hivyo ni MAMCU Ltd na TANECU Ltd kutoka Mkoa wa Mtwara, RUNALI Ltd na LMCU Ltd kutoka Mkoa wa Lindi, TAMCU Ltd kutoka Mkoa wa Ruvuma na CORECU Ltd kutoka Mkoa wa Pwani. Kampuni hii inatekeleza shughuli zake hususani uagizaji wa pembejeo kwa kuzingatia taratibu, miongozo, kanuni na sheria zilizopo nchini chini ya usimamizi wa karibu wa CBT, TCDC, TARI Naliendele na TPHPA.

Zoezi la kuwapata na kufunga mkataba na wazabuni lilianza Oktoba, 2023 baina ya KCJE Ltd ambapo wazabuni 17 walifunga mkataba kwa ajili ya kusambaza pembejeo sulphur ya unga tani 30,000, viuatilifu vya maji lita 3,800,000.

## 6.0 UDHIBITI WA UBORA WA PEMBEJEO

Udhibiti wa ubora wa pembejeo utazingatia taratibu, miongozo, kanuni na sheria za TPHPA. Aidha, kwa lengo la kujiridhisha na ubora wa pembejeo kabla ya kusambazwa kwa wakulima, KCJEL itachukua sampuli kwa kila toleo *(Batch No.)* la viuatilifu na kuzipeleka kupimwa TPHPA. Pembejeo zitakazokidhi ubora kwa taarifa rasmi toka TPHPA ndizo zitakazosambazwa kwa wakulima na zile zitakazokuwa chini ya kiwango hazitasambazwa kwa wakulima.

Sambamba na hilo, TARI Naliendele kwa kushikirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania na Halmashauri imeteua mashamba ya mfano yatakayotumika kama mashamba darasa kwenye kila Halmashauri shamba moja lisilozidi ekari 1 kutoka kwa mkulima kwa kuzingatia jiografia ya kanda zinazolima korosho nchini katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani. Mashamba ya mfano yatatumia pembejeo zinazotolewa na Serikali kwa wakulima nchini kwa ajili ya kuonesha kwa vitendo juu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu vinavyotolewa kwa ruzuku na Serikali.

## 7.0 GHALA KUU ZA PEMBEJEO

Ili kupunguza gharama za usafirishaji kutoka ghala kuu kwenda kwa wakulima, ghala kuu zimeandaliwa kwenye kila Mkoa ambapo kwa Mkoa wa Mtwara zitakuwa katika Halmashauri za Mtwara Mikindani, Tandahimba na Masasi TC; Lindi zitakuwa kwenye Manispaa ya Lindi; Pwani zitakuwa Halmashauri ya Kibiti na Ruvuma Halmashauri ya Tunduru. Ghala Kuu zote zitakuwa chini ya uendeshaji wa Meneja Dhamana wa Kampuni ya *ACE*

*Global Depository (Tanzania) Ltd* atakayefanya kazi chini ya usimamizi wa CBT kwa kushirikiana na KCJE Ltd.

Ghala Kuu za Mtwara Mikindani, Tandahimba na Masasi TC zitapokea na kuhifadhi pembejeo za Mkoa wa Mtwara; Ghala Kuu la Manispaa ya Lindi litapokea na kuhifadhi pembejeo za Mkoa wa Lindi; Ghala Kuu la Tunduru Mjini litapokea na kuhifadhi pembejeo za Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya na Songwe; na Ghala Kuu la Kibiti Mjini litapokea na kuhifadhi pembejeo za Mikoa ya Pwani, Tanga na mikoa mipya iliyobaikia.

## 8.0 USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO

Wazabuni watasafirisha pembejeo hadi kwenye ghala kuu kadri watakavyoelekezwa na KCJE Ltd kwa kushirikiana na CBT. Jukumu la kusafirisha pembejeo kutoka ghala kuu kwenda vituo vya kugawa pembejeo kwa wakulima katika mikoa ya asili litakuwa chini ya KCJEL kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika. Kwa upande wa mikoa mipya Halmashauri husika kwa kushirikiana na CBT watahusika.

## 9.0 MFUMO WA KIDIJITALI WA UGAWAJI WA PEMBEJEO

Mfumo utakaotumika kugawa viuatilifu kwa wakulima msimu wa 2024/2025 ni wa kielektroniki utakaotumia *Application* maalum ya kidigitali *(Digital App.)*. *Application* hiyo itaratibiwa na kusimamiwa na CBT. Kupitia utaratibu huo, wadau muhimu wakiwemo wakulima, AMCOS, Vyama Vikuu vya Ushirika, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na CBT watasajiliwa. Aidha, mfumo huu utaratibu takwimu za usambazaji *(Stock movement)* na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima kupitia *QR code* zitakazoambatana na pembejeo wakati wa usambazaji sanjari na kutoa takwimu za viuatilifu vilivyopokelewa; vilivyosambazwa na vilivyomo kwenye ghala la kituo cha ugawaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima.

## 10.0 USAJILI WA VITUO VYA KUGAWA PEMBEJEO

CBT kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na Vyama Vikuu vya Ushirika itasajili vituo vitakavyotumika kupokea na kugawa pembejeo kwa wakulima. Vituo hivi ni AMCOS zenye ghala zinazokidhi viwango na pia miundombinu ya barabara inayofikika kwa urahisi pamoja na upatikanaji wa mtandao wa *internet*. Aidha, ili kuwa na ufanisi wakati wa usimamizi na ufuatiliaji, vituo kulingana na jiografia ya maeneo yanayolima korosho ndani ya Halmashauri husika vitahusika pasipo kuathiri ghala zilizotengwa kwa ajili ya ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya ufuta na mbaazi.

### 10.1. UTARATIBU WA UGAWAJI WA PEMBEJEO

### 10.2. Usajili/Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Korosho

Ugawaji wa pembejeo kwa wakulima utafanyika kwa wale watakaokuwa wamesajiliwa kupitia njia moja wapo kati ya hizi zifuatazo:

i. Mfumo wa kigijitali kupitia *CBT Tool App*. Mfumo huo utakuwa na taarifa muhimu zikiwemo idadi wa mikorosho, ukubwa wa shamba na picha ya mkulima na hatimaye kutoa namba maalum *(Unique number)* itakayotumika kumtambua mkulima atakayepokea pembejeo kupitia Neno Siri la Maramoja *(One Time Password (OTP))*; na
ii. Kupitia Kitabu/Daftari Maalumu la Usajili kwa Wakulima kwa Mikoa ambayo haijafikiwa na zoezi la usajili kwa kutumia mfumo kidijitali.

***MUHIMU: Namba maalum pamoja na OTP itatumika kama utambulisho wa mkulima wakati wa kupata huduma ya pembejeo za ruzuku za korosho msimu wa mwaka 2024/2025.***

### 10.3. Mgao na Ugawaji wa Pembejeo kwa Wakulima

Mgao wa pembejeo za ruzuku hususani viuatilifu utazingatia takwimu za usajili wa wakulima ambazo ni idadi ya miti ya mikorosho iliyohuishwa kwenye kanzidata. Hata hivyo, kutokana na mahitaji halisi ya pembejeo kwa wakulima kutoendana na mpango wa ruzuku wa Serikali, uwiano kutoka kwenye takwimu hizo utatumika kuandaa mgao halisi wa viuatilifu kwa mkulima mmoja mmoja kwa kuzingatia idadi ya mikorosho kama ilivyotajwa hapo juu.

***Kwa mantiki hiyo, wakulima wanakumbushwa kwamba ruzuku inayotolewa na Serikali ni mchango wake katika kumpunguzia mkulima gharama za kuzalisha korosho. Kila mkulima anapaswa kuweka akiba ya fedha kwa ajili ya shughuli za maandalizi ya shamba ikiwemo kununua viuatilifu sokoni vya kutosheleza mahitaji***.

Kwa upande wa utaratibu wa ugawaji, Wakulima wote waliosajiliwa watatakiwa kwenda katika vituo vilivyopo ndani ya kata wanapoishi kwa ajili ya kupokea mgawo wakiwa na **Namba ya Utambulisho wa Mkulima *(Farmer Identity Number – Farmer ID)*** pamoja na **Kitambulisho cha Mpiga Kura** au **Kitambulisho cha Utaifa (NIDA) au Leseni ya Udereva** kwa ajili ya uhakiki wa taarifa za mkulima kabla ya kukabidhiwa mgao wake. Kwa wakulima wasio na kitambulisho watatakiwa kupata barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji chake kwa ajili ya kumtambulisha ili aweze kupatiwa huduma ya pembejeo. Inasisitizwa mkulima kufika mwenyewe kuchukua mgawo wake hivyo ni marufuku kwa mkulima kumchukulia mkulima mwenzake mgawo wake na kwa yeyote atakayebainika hatua zitachukuliwa dhidi yake.

Katibu/karani wa AMCOS atatakiwa kuhakiki namba ya mkulima kabla ya kumpatia huduma na baada ya kujiridhisha kuwa taarifa zake zinaendana na zile zilizopo kwenye kitambulisho cha NIDA au Mpiga Kura au Barua ya Utambulisho kutoka Ofisi ya Kijiji ataingiza namba ya mkulima kwenye mfumo na mkulima atapata ujumbe mfupi papo hapo (*One Time Password – OTP*) ukimtaka kuweka nywila au neno la siri kwenye simu yake ili kukiri na kukamilisha taratibu za kupata mgao wake. Kwa Mkulima ambaye namba yake ya simu itakuwa imekosewa atatakiwa kuwasiliana na Bodi ya Korosho Tanzania kupitia namba ya simu ya bure ambayo ni 0800112159 akiwa na Barua ya Utambulisho kutoka Ofisi ya Kijiji kwa ajili ya kurekebisha taarifa zake katika namba yake ya simu.

***MUHIMU: Ikumbukwe kuwa mkulima asiye na namba ya simu (Line) hataweza kupata mgao wake wa pembejeo.***

## 11.0 JINSI MFUMO WA KIDIJITALI UTAKAVYOFANYA KAZI

Usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho kwa mfumo wa kidijitali katika msimu wa mwaka 2024/2025 utazingatia utaratibu ufuatao:-

i. Wazabuni wataingiza pembejeo nchini kwa mujibu wa mikataba baina yao na KCJE Ltd. Pembejeo hizo zitawasilishwa kwenye ghala kuu zilizopo mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma ambazo zipo chini ya usimamizi wa Meneja Dhamana wa Kampuni ya *ACE Global Depository (Tanzania) Ltd*;

ii. Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika na Halmashauri husika zitasajili vituo vya ugawaji wa pembejeo kwa wakulima;

iii. Wakulima watasajiliwa kwenye kanzidata ya kielektroniki na kupatiwa namba maalum ambazo watazitumia kupata huduma ya pembejeo kwenye ghala za AMCOS;

iv. Majina ya wakulima waliosajiliwa yatabandikwa kwenye Ofisi za Serikali za Vijiji na AMCOS ndani ya eneo husika;

v. Vyama Vikuu vya Ushirika vitasafirisha pembejeo kutoka ghala kuu kwenda AMCOS;

vi. AMCOS itatumia mfumo wa kidijitali ulioandaliwa na Bodi ya Korosho kugawa pembejeo; na

vii. Kwa upande wa mabomba, hayatasambazwa kwa njia ya mfumo wa ugawaji pembejeo isipokuwa kwa mkulima atakayehitaji bomba la kupulizia atatakiwa kuchangia nusu ya gharama kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3** hapo chini.

**Jedwali Na. 3: Bei ya soko ya bomba na nusu yake ambayo mkulima anatakiwa kuchangia.**

| Na. | Mzabuni | Chapa ya Bomba | Bei ya Soko (Tshs.) | Nusu ya Bei ya Soko (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Meru Agro | Pulmic take control | 1,195,000.00 | 597,500.00 |
| 2 | Faham Africa | Shogun | 780,000.00 | 390,000.00 |

## 12.0 UTOAJI WA ADHABU

Utekelezaji wa Mwongozo huu utazingatia sheria za Tanzania ikiwemo Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010; Wadau wote wanapaswa kuzingatia Sheria za nchi ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Mwongozo huu. Vitendo vyovyote vya ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu au vitakavyobainika kuwa na lengo la kukwamisha utaratibu wa ugawaji wa pembejeo kwa mtu yeyote hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

## 13.0 USIMAMIZI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Jukumu la kusimamia na kufuatilia mwenendo wa zoezi zima la usambazaji wa pembejeo ni la ngazi zote kuanzia Serikali Kuu, Mikoa na Wilaya. Aidha, ili kuwa na ufanisi kutakuwa na Kamati ya Kitaifa ambayo chini yake kila Mkoa na Wilaya utakuwa na kikosi kazi cha kusimamia na kufuatilia mwenendo nzima wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima katika mkoa husika.

### 13.1. Muundo wa Kamati ya Kitaifa

Kamati ya Kitaifa ya usimamizi na ufuatiliaji wa usambazaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho kwa wakulima msimu wa 2024/2025 itahusisha taasisi za serikali kama ifuatavyo:

i. Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania – Mwenyekiti;
ii. Bodi ya Korosho Tanzania – Sekretarieti ya Kamati;
iii. Kampuni ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika – Mjumbe;
iv. Usalama wa Utaifa Mkoa wa Mtwara – Mjumbe;
v. Jeshi la Polisi Mkoa wa Mtwara – Mjumbe;
vi. TAKUKURU Mkoa wa Mtwara – Mjumbe;
vii. Wawakilishi watatu Vyombo vya Ulinzi na Usalama – Wajumbe;
viii. TARI Naliendele – Mjumbe;
ix. Mwakilishi mmoja toka Sekretarieti za Mikoa – Mjumbe;
x. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania – Mjumbe;

***MUHIMU: Kamati hii itakuwa ikikutana kila baada ya wiki mbili katika kipindi chote cha usambazaji kwa lengo la kupokea na kupitia taarifa za utekelezaji wa zoezi la usambazaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho msimu wa mwaka 2024/2025.***

### 13.2. Muundo wa Kikosi Kazi cha Mkoa

Kikosi kazi cha Mkoa kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima msimu wa 2024/2025 ndani ya Mkoa kitahusisha:

i. Sekretarieti ya Mkoa – Mwenyekiti na Katibu;
ii. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa – Mjumbe;
iii. Mwakilishi mmoja kutoka kila *Union* – Mjumbe; na
iv. TAKUKURU Mkoa – Mjumbe.

### 13.3. Muundo wa Kikosi Kazi cha Wilaya

Kikosi kazi cha wilaya kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima msimu wa mwaka 2024/2025 ndani ya wilaya kitahusisha:

i. Wajumbe wa kamati ya pembejeo ya Wilaya; na
ii. Mwakilishi wa chama kikuu cha ushirika.

## 14.0 UGHARAMIAJI KWA WANAOHUSIKA NA USIMAMIZI NA UFUATILIAJI

Kwa kuwa wahusika katika shughuli za usambazaji wa pembejeo kwa namna moja ama nyingine ni wanufaika *(Beneficiaries)* wa zao la korosho hapa nchini; kila kamati itatakiwa kujigharamia ili kuweza kufikia malengo ya uzalishaji wa korosho ghafi tani 595,000 msimu wa 2024/2025 na tani 700,000 ifikapo mwaka 2025/2026.

## 15.0 UGHARAMIAJI WA SHUGHULI ZA USAMBAZAJI NA UGAWAJI

Shughuli ya usafirishaji wa pembejeo kutoka ghala kuu kwenda Vyama vya Msingi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha usalama wa mzigo na gharama zote zinazohusika zitalipwa na KCJEL Ltd kwa kushirikiana na *Unions*. Kwa upande wa shughuli ya ulinzi na ugawaji kwa wakulima katika ngazi ya AMCOS zitalipwa na AMCOS husika. Aidha, shughuli zote za AMCOS zitafanyika chini ya usimamizi wa Vyama Vikuu vya Ushirika wakishirikiana Mrajis Msaidizi wa Mkoa na Afisa Ushirika wa Halmashauri husika.

## 16.0 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

Endapo kutatokea malalamiko yoyote juu ya usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho yawasilishwe na kushughulikiwa kulingana na ngazi za utekelezaji kuanzia AMCOS, Halmashauri, Chama Kikuu cha Ushirika, Wilaya, Mkoa na Bodi ya Korosho Tanzania. Aidha, Bodi ya Korosho Tanzania imeandaa namba ya simu ya bure ambayo ni ***0 8 0 0 1 1 2 1 5 9*** kwa ajili ya kupokea maoni, ushauri malalamiko na kuyashughulikia kulingana na ngazi husika.

## 17.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU

Ili kuhakikisha zoezi la ugawaji wa pembejeo na mabomba katika zao la korosho msimu wa 2024/2025 linafanikiwa, majukumu ya kiutendaji na kitaasisi yamegawanywa kama ilivyoelezwa hapo chini:-

### 17.1. Wizara ya Kilimo

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia mpango wa ruzuku ya pembejeo za zao la korosho;
(ii) Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya ununuzi na usambazaji wa pembejeo, mabomba na magunia katika zao la korosho;
(iii) Kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kulipia gharama ya pembejeo zitakazosambazwa kwa wakulima; na
(iv) Kushughulikia masuala mengine yatakayohitaji maamuzi ya Wizara juu ya pembejeo za ruzuku za zao la korosho.

### 17.2. Kikosi Kazi cha Mkoa

(i) Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania katika kusimamia na kuhamasisha wakulima kujisajili ikiwa ni pamoja na kuhuisha taarifa zao zilizopo kwenye kanzidata;
(ii) Kuratibu mgao wa pembejeo na mabomba ya zao la korosho kwenye Halmashauri ndani ya Mkoa;
(iii) Kushirikiana na TPHPA, TARI Naliendele, TCDC na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(iv) Kuratibu shughuli za kikosi kazi cha Mkoa kwenye usimamizi na ufuatiliaji wa zoezi la usambazaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho;
(v) Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka utaratibu wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika; na

(vi) Kuhakikisha uwepo wa vituo vya kugawa pembejeo kwa wakulima kupitia AMCOS;
(vii) Kuwa na akaunti ya usajili nausambazaji pembejeo ili kuona zoezi na kusaidia wakulima.

### 17.3. Bodi ya Korosho Tanzania

(i) Kuhuisha na kusajili wakulima wa zao la korosho nchini;
(ii) Kuunda na kuratibu utendaji kazi wa Kamati ya Kitaifa usimamizi na usambazaji wa pembejeo za ruzuku;
(iii) Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya pembejeo, mabomba na magunia iliyofungwa kati ya wazabuni na KCJEL;
(iv) Kuhakikisha pembejeo, mabomba na magunia yanasambazwa kwa wakulima kwa kuzingatia taratibu;
(v) Kufuatilia, kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza taarifa zinazohusu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za zao la korosho;
(vi) Kupokea hati za maombi ya malipo ya pembejeo za ruzuku zilizosambazwa kuhakiki taarifa za usambazaji kwa mujibu wa mkataba na kushughulikia taratibu za malipo kwa maombi yatakayowasilishwa;
(vii) Kuratibu mafunzo ya mfumo wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa AMCOS zilizoteuliwa kutekeleza shughuli hiyo;
(viii) Kushirikiana na TPHPA, TARI Naliendele, TCDC, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(ix) Kusimamia utekelezaji wa mwongozo huu katika ngazi zote na kuchukua hatua za kiutendaji; na
(x) Kutengeneza akaunti ya kila Mkoa na Halmashauri kwa ajili ya kuona mwenendo wa usajili wa wakulima na usambazaji wa pembejeo unavyoenenda;

### 17.4. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

(i) Kutoa waraka unaoainisha wajibu wa Vyama vya Ushirika husika kutekeleza maelekezo ya Serikali juu ya uagizaji na usambazaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima msimu wa 2024/2025;
(ii) Kuvielekeza vyama vikuu vya ushirika kuwawezesha Makatibu wa AMCOS kushiriki kwenye mafunzo ya mfumo wa usambazaji wa pembejeo, kusimamia ugawaji wa pembejeo na ulinzi wa pembejeo ziwapo kwenye vituo vya kugawa pembejeo;

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya pembejeo, mabomba na magunia iliyofungwa kati ya wazabuni na KCJEL;
(iv) Kushirikiana na Bodi ya Korosho, TPHPA, TARI Naliendele, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(v) Kufuatiliana na kusimamamia mwenendo wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kutoka vyama vya ushiriki kwenda kwa wakulima.

**17.5. Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri)**

(i) Kukusanya taarifa za makadirio ya mahitaji ya pembejeo kutoka kwa wakulima;
(ii) Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kusajili na kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho;
(iii) Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kusajili vituo (AMCOS) vya kugawa pembejeo kwa wakulima;
(iv) Kushirikiana na Bodi ya Korosho, TCDC, TPHPA, TARI Naliendele na Sekretarieti za Mikoa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(v) Kufuatilia na kusimamamia mwenendo wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kutoka vyama vya ushiriki kwenda kwa wakulima;
(vi) Kusimamia AMCOS hususani wakati wa mapokezi, usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima;
(vii) Kusimamia na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya pembejeo kwa wakulima;
(viii) Kuwasaidia wakulima waliopoteza namba ya mkulima kupata namba zao; na
(ix) Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka taratibu za ugawaji wa pembejeo ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwenye mamlaka husika.

**17.6. Vyama Vikuu vya Ushirika**

(i) Kufanya manunuzi ya pembejeo, mabomba na magunia kupitia Kampuni ya Pamoja kwa kuzingatia taratibu, miongozo, kanuni na sheria zilizopo kupitia kampun ya KCJE Ltd;
(ii) Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya pembejeo, mabomba na magunia iliyofungwa kati ya wazabuni na KCJEL;
(iii) Kuandaa nyaraka za mapokezi na usambazaji wa pembejeo, mabomba na magunia;
(iv) Kushirikiana na Bodi ya Korosho, TPHPA, TARI Naliendele na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na

kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;

(v) Kuandaa ghala za kupokelea pembejeo, mabomba na magunia kutoka ghala kuu kwenda kwa wakulima;

(vi) Kupokea pembejeo, mabomba na magunia kutoka kwa wazabuni;

(vii) Kushirikiana na KCJEL kusafirisha pembejeo, mabomba na magunia kutoka ghala kuu kwenda vituo vya ugawaji;

(viii) Kusimamia usambazaji na ugawaji wa pembejeo, mabomba na magunia katika eneo husika;

(ix) Kutunza kumbukumbu zote za uagizaji, usambazaji na ugawaji wa pembejeo, mabomba na magunia katika eneo la chama husika;

(x) Kupitia na kuhakiki nyaraka/ankara za madai kwa lengo la kujiridhisha na usahihi wake kabla ya kuwalipa wazabuni; na

(xi) Kuwa na akaunti za usajili na usambazaji ili kuweza kuona na kusaidia wakulima

(xii) Kusimamia usafirishaji, upakiaji na ushushaji wa viuatilifu kwenye hadi AMCOS

### 17.7. Vyama vya Ushirika vya Msingi

(i) Kusajili ghala litakalotumika kupokea na kugawa pembejeo, mabomba na magunia;

(ii) Kupokea mafunzo ya mfumo wa ugawaji wa pembejeo na mabomba;

(iii) Kupokea pembejeo na kugawa kwa wakulima kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa;

(iv) Kutunza kumbukumbu za pembejeo zilizopokelewa na kugawiwa kwa wakulima.

(v) Kabla ya mkulima kukabidhiwa mgawo wake kwenye mfumo aoneshwe kabla ya kujiridhisha.

(vi) Kuandaa mabango ya wakulima walionufaika na magawo wa pembejeo na kubandika kwenye bao za matangazo;

### 17.8. TARI Naliendele

(i) Kuthibitisha na kufuatilia matumizi sahihi ya pembejeo husika kwenye zao la korosho;

(ii) Kushirikiana na Bodi ya Korosho, TCDC, TPHPA, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;

(iii) Kufuatilia mwenendo wa uzalishaji wa korosho na hali ya hewa na kutoa ushauri wa kitaalam juu matumizi ya viuatilifu;

(iv) Kutoa mapendekezo ya pembejeo na mabomba yanayofaa kuagizwa na kusambazwa kwa wakulima;
(v) Kutoa ushauri wa kitaalam kwenye Kamati ya Ununuzi wa Pamoja wa pembejeo, mabomba na magunia; na
(vi) Kushirikiana na CBT, TPHPA kuendesha mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima.

**17.9. KCJEL Ltd**

(i) Kulipa wazabuni na watoa huduma wengine kwa kuzingatia mikataba;
(ii) Kusaini mikataba na wazabuni wa usambazaji wa pembejeo, mabomba na magunia;
(iii) Kusimamia utekelezaji wa mikataba ulioingiwa na wazabuni;
(iv) Kuandaa ghala kuu za mapokezi ya pembejeo, mabomba na magunia kutoka kwa wazabuni kabla ya kusambazwa kwenda kwa wakulima;
(v) Kutafuta ghala za kuhifadhi pembejeo, kulipa washushaji na wapakiaji pamoja na wasafirishaji kutoka ghala kuu kwenda ghala za AMCOS; na
(vi) Kutafuta na kuingia mikataba na wasafirishaji wa pembejeo kutoka ghala kuu kwenda ghala za AMCOS kwa ajili ya kusambazwa.

**17.10. Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania**

(i) Kuainisha viambata amilifu (Active ingredients) kwenye viuatilifu vya zao la korosho kwa lengo la kulinda viwango na ubora;
(ii) Kushirikiana na Bodi ya Korosho, TCDC, TARI Naliendele, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(iii) Kufanya ukaguzi mara kwa mara wa viuatilifu vya korosho vinavyotumika nchini na kuchukua hatua pale sheria husika inapokiukwa;
(iv) Kujiridhisha na ubora wa viuatilifu vyote kabla ya kusambaza kwa wakulima.

**17.11. Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Pembejeo za Ruzuku za Korosho**

(i) Kujiridhisha na ubora wa pembejeo kabla ya kukabidhiwa kwa Vyama Vikuu vya Ushirika;

(ii) Kufuatilia zoezi la mapokezi, usambazaji na ugawaji wa pembejeo na magunia kwenye ghala kuu; na
(iii) Kushirikiana na Bodi ya korosho na wadau wengine kudhibiti mianya yoyote ya ubadhirifu inayoweza kuibuka wakati wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima.
(iv) Kuchukua hatua dhidi ya vitendo vyovyote vya ukiukwaji wa mwongozo huu,
(v) Kusimamia na kufuatilia zoezi zima la mapokezi na usambazaji;
(vi) Kuandaa taarifa kuu ya mapokezi na usambazaji

### 17.12. Kikosi Kazi cha Wilaya

i. Kusimamia na kufuatilia zoezi zima la ugawaji wa pembejeo kwa wakulima katika ngazi ya wilaya; na
ii. Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka taratibu za ugawaji wa pembejeo.

### 17.13. Wazabuni wa Pembejeo

i. Kuagiza na kusambaza pembejeo kwa mujibu wa mkataba baina yake na Kampuni ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika;
ii. Kuingiza Viuatilifu vinavyokidhi viwango vya ubora kwa kuzingatia mwongozo, heria na matakwa ya mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA).
iii. Kuwasilisha kwa Bodi ya Korosho Tanzania na TCDC nakala za nyaraka za makabidhiano ya viuatilifu aliyoyafanya kwa Kampuni ya Pamoja;
iv. Kuwasilisha Bodi ya korosho nyaraka za idhini za ubora wa viuatilifu alivyoagiza toka TPHPA kabla ya kupokelewa na KCJE Ltd na kusambazwa kwa mujibu wa mwongozo huu
v. Kuwasilisha hati za madai kwa Kampuni ya KCJE Ltd;
vi. Kugharamia mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya pembejeo yanayoratibiwa na Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele; na
vii. Kuhamasisha wakulima juu ya matumizi sahihi na salama ya pembejeo zinazosambazwa kwa mujibu wa mkataba baina yake na Kampuni ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika.
viii. Kujiepusha na vitendo vya udanganyifu na ukiukwaji wa sheria na mwongozo huu

### 17.14. Mkulima wa Korosho

i. Kuhakikisha kuwa amesajiliwa na amehuisha taarifa zake kwenye kanzidata ya wakulima wa korosho iliyopo Bodi ya Korosho Tanzania;
ii. Kuhakikisha kuwa shamba lake ni safi;
iii. Kusaini fomu ya kukiri kuchukua pembejeo wakati wa kukabidhiwa pembejeo;
iv. Kutumia pembejeo kwa usahihi, yaani kutimiza idadi ya mipulizo inayotakiwa na kutumia viwango na vipimo sahihi kama inavyoelekezwa na mtaalam wa kilimo (Afisa Kilimo) aliyepo katika eneo lake;
v. Kutunza kumbukumbu za matumizi ya pembejeo kwa kuandika kwenye daftari na kutunza nyaraka za uchukuaji wa viuatilifu na mabomba kutoka kwenye Kamati ya Pembejeo ya Kijiji;
vi. Hairuhusiwi kutumia namba ya mkulima zaidi ya moja kupata huduma za pembejeo;
vii. Haruhusiwi kuuza wala kununua pembejeo za bure zinazotolewa na Serikali;
viii. Kutoa taarifa kwa Afisa Kilimo wa Kata juu ya ukiukwaji wowote wa Mwongozo;
ix. Hakikisha umesaini fomu ya kukiri kupokea viuatilifu.

### 17.15. Taasisi za Fedha

i. Kutoa huduma za kifedha kwa wadau wa korosho nchini ikiwa ni pamoja na wakulima na wazabuni wa pembejeo; na
ii. Kutoa elimu ya huduma za kifedha kwa wadau wa korosho ikiwa ni pamoja na wakulima na wazabuni wa pembejeo.

### 17.16. Waandishi wa Habari

i. Kuhabarisha umma juu ya taarifa za upatikanaji, usambazaji, ugawaji na matumizi ya pembejeo za korosho.
ii. Kuhakikisha wanatoa taarifa sahihi za utekelezaji wa mwongozo huu

## 18.0 WAJIBU WA PAMOJA

i. Kuhakikisha majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia sera na sheria za
ii. nchi;
iii. Kutoa taarifa mapema kuhusu suala lolote ambalo litakwamisha utekelezaji wa mpango huu.

iv. Kuhakikisha pembejeo zinamnufaisha mkulima akiwa mtumiaji wa mwisho na sio mtu wa kati au asiye mlengwa wa utaratibu wa ugawaji pembejeo za ruzuku.
v. Kuhakikisha kila mdau husika anatimiza wajibu wake.

## 19.0 MUDA WA UTEKELEZAJI

Mwongozo huu utatekelezwa kipindi chote cha mapokezi na usambazaji wa pembejeo za msimu wa 2024/2025.

## 20.0 ILANI

Serikali haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa mdau ambaye hatazingatia utaratibu uliowekwa kwenye Mwongozo huu.

## 21.0 HITIMISHO

Serikali imeamua kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo za korosho kwa wakulima wa zao la korosho nchini ili waweze kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi. Hii ni kutokana na mchango mkubwa wa zao la korosho kwenye pato la mkulima na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, ni wajibu wa wadau wote wanaohusika kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali inahimiza ushirikiano wa wadau katika ngazi zote ili kuhakikisha kuwa mpango huu wa ruzuku unatekelezwa kwa ufanisi. Mwisho, Mwongozo huu unaweza kufanyiwa maboresho wakati wowote kulingana na mahitaji kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku.

Mwongozo huu umetolewa na kusainiwa leo tarehe ...18... **Aprili, 2024**

Francis Alfred
**Mkurugenzi Mkuu**
Bodi ya Korosho
Tanzania